

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA MITIHANI
MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A

661

SAIKOLOJIA YA ELIMU NA KUNASIHI

MUDA: Saa 3

2006/10/10 Asubuhi

Maelekezo

1. Karatasi hii ina sehemu A, B na C.
2. Jibu maswali yote kutoka sehemu A, maswali mawili (2) kutoka sehemu B na swali moja (1) kutoka sehemu C.
3. Sehemu A ina alama 36, sehemu B ina alama 40 na sehemu C ina alama 24.
4. Simu za mkononi haziruhusiwi kwenye chumba cha mtihani.
5. Andika Namba yako ya Mtihani katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

SEHEMU A (alama 36)
Jibu maswali yote kutoka shemu hii.

1. Swali limejengwa kwa mafungu mawili. Fungu M ni sehemu tu ya wazo kamili lililokusudiwa, ambalo litakamilika kwa kuoanishwa na sehemu ya pili ya wazo hilo, iliyopo kwenye fungu J. andika herufi A, B, C, D, E na F ya fungu M ikifuatwa na jibu sahihi kutoka fungu J.

M	J
A Tendo la kujifunza linaweza kutokea kwa kufuata kanuni muhimu zinazofanikisha tendo hilo. <i>kujifunza sana na stadi</i>	- Maarifa, mwelekeo na stadi. <i>C</i>
B Tendo la kuoanisha mafunzo ya awali ili kuendeleza na kufanikisha mafunzo mapya. <i>Kuhautisha mafunzo</i>	- Aina za kujifunza. <i>A</i>
C Nyanja za kujifunza. <i>maarifa mwelekeo stadi</i>	- Kusahau.
D Uzoeshi, kuiga, kumaizi. <i>Aina za kujifunza</i>	- Vurugu za maono zilizoambatana na hasira, woga au wivu.
E Kushindwa kurejesha akilini wazo fulani ulilokuwa unalijua, bila mafanikio. <i>Kusahau</i>	- Chanya na hasi
F Mambo yanayoweza kuathiri kukumbuka. <i>vurugu za maono</i>	- Utayari, mazoezi, matokeo.
	- Kuhawilisha mafunzo. <i>B</i>
	- Kuhamisha mafunzo.
	- Hizo ni kanuni za uzoeshi.
	- Kujifunza sana na kupewa mazoezi mengi.

2. Toa maana ya saikolojia ya elimu.
3. Bainisha mambo **matatu (3)** ambayo mtoto wa mwaka mmoja hadi miwili anaweza kuyamudu.
4. Dhana ya "akili iliyovia" ina maana gani?
5. Eleza mambo muhimu **matatu (3)** ambayo yanasaidia kuifafanua zaidi dhana ya kanuni ya utambuzi katika kujifunza.
6. Ikiwa mtoto ana umri wa miaka mitano (5) ya kuzaliwa, na wakati huo anao uwezo wa akili sawa na mtoto mwingine mwenye umri wa miaka 6, tafuta hisa ya akili.
7. Kwa kutoa mifano, bainisha tofauti iliyopo kati ya motisha shauku na motisha kishawishi.
8. Bainisha faida **tatu (3)** za kucheza michezo shuleni.
9. Taja hatua **tatu (3)** za kiutendaji katika nyanja ya stadi

*20
6
120*

SEHEMU B (alama 40)
Jibu maswali mawili (2) kutoka sehemu hii.

10. Kwa kutoa mifano, eleza umuhimu wa mwalimu mwanafunzi kufundisha saikolojia ya elimu na kunasihii. Toa hoja tano (5).
11. (a) Kwa kutumia hoja tatu (3), eleza dalili ambazo uzionapo darasani wakati wa kufundisha, zinaweza kuashiria kuwa mwanafunzi husika ana matatizo ya kuona; Vilele
(b) Eleza hatua utakazochukua ili kuwasaidia watoto wenye matatizo kama hayo darasani.
12. Eleza hatua nne (4) za ukuaji wa mtoto kiakili, kulingana na mawazo ya mwanasaikolojia Jean Piaget (1896 – 1980).
- * 13. Fafanua kanuni tatu (3) za kujifunza kama zilivyoelezwa na E. Thorndike.

SEHEMU C (alama 24)
Jibu swali moja (1) kutoka sehemu hii.

14. Eleza mambo manne (4) ambayo uwepo wake husaidia kufanikisha tendo la uhawilishaji wa mafunzo kufanikiwa. *Kutambambina wote wanafunzi kutoa wachanganyo wake*
kuwashiriki kisher wanafunzi
kuta mwa zana
15. Makuzi ya mtoto huanza tangu kutunga kwa mimba ndani ya tumbo la uzazi la mama. Eleza mambo mawili (2) kwa kila kipengele ambayo wazazi wakiyatenda, hufanikisha kukua vizuri kiakili, kimwili na kimaono.
16. Kwa kurejea mtaalamu aitwaye Bloom, tunga maswali mawili (2) kwa kutumia mada yoyote kwa kila stadi ya nyanja ya utambuzi katika malengo ya kielimu. Stadi zinazohusika ni:
- (a) Maarifa
 - (b) Ufahamu
 - (c) Matumizi
 - (d) Uchanganuzi
 - (e) Unganisho
 - (f) Tathmini.

kushindwa kushiriki kwenye vitendo mbalimbali
kushindwa kusoma na kuandika
kutoa kushiriki kati ka michezo mbalimbali